**HOTUBA YA KWANZA.**

**حسن العشرة وحفظها**

**KUISHI KWA WEMA NA KUULINDA**

**Imefasiriwa**

**Na**

**Profesa Ayman Alasar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote. Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake:

**فَبِمَا رَحْمَةٍ مِنَ اللَّهِ لِنْتَ لَهُمْ وَلَوْ كُنْتَ فَظًّا غَلِيظَ الْقَلْبِ لَانْفَضُّوا مِنْ حَوْلِكَ**

{**Basi ni kwa sababu ya rehema itokayo kwa Mwenyezi Mungu ndio umekuwa laini kwao. Na lau ungeli kuwa mkali, mwenye moyo mgumu, bila ya shaka wangeli kukimbia**}.

Ninashuhudia kuwa hakua mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika. Na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni Mja wake na Mtume wake. Ewe Mwenyezi Mungu tunaomba peleka rehma na amani kwake pamoja na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake na kwa wale wote waliomfuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

**Baada ya utangulizi**:

Mashirikiano mema pamoja na kuyalinda ni katika tabia na maadili mazuri ambayo dini yetu ya Uislamu imelingania kwenye hilo, pia ni katika mwenendo wa waja wema waaminifu, ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu Anasema:

**وَأَحْسِنُوا إِنَّ اللهَ يُحِبُّ الْمُحْسِنِينَ.**

{**Na fanya wema hakika Mwenyezi Mungu anawapenda wafanyao wema**}. Na Anasema tena Mola Mtukufu: **وَلَا تَنْسَوُا الفَضْلَ بَيْنَكُم** {**Wala msisahau mazuri na**

**mema mnayofanyia kati yenu**}. Na akasema tena: **هَلْ جَزَاء الْإِحْسَانِ إِلَّا الْإِحْسَانُ** {**Ati yaweza kuwa malipo ya wema isipokwa ni wema**}. Na Mtume S.A.W anasema:

**وَمَنْ آتَى إِلَيْكُمْ مَعْرُوفًا فَكَافِئُوهُ، فَإِنْ لَمْ تَجِدُوا فَادْعُوا لَهُ حَتَّى تَعْلَمُوا أَنْ قَدْ كَافَأْتُمُوهُ.**

"***Atakapowajieni mtu mwema basi mlipeni kwa wema wake, na ikiwa hamna cha kumlipa au kizuri cha kumfanyia basi muombeeni duwa ili afahahmu kuwa mumemfanyia wema***".

Mwenye kuzingatia mwenendo wa Mtume S.A.W atakuta mfano mzuri wa kuigwa katika kuishi kwake vizuri na watu wa nyumbani kwake ndugu zake na Maswahaba zake pamoja na watu wote, kwani Mtume ndiye aliyesifiwa na Mola wake kwa kauli yake:

**لَقَدْ جاءَكُمْ رَسُولٌ مِنْ أَنْفُسِكُمْ عَزِيزٌ عَلَيْهِ ما عَنِتُّمْ حَرِيصٌ عَلَيْكُمْ بِالْمُؤْمِنِينَ رَؤُفٌ رَحِيمٌ.**

{**Hakika amekwisha kujieni Mtume kutokana na nyinyi wenyewe; yanamhuzunisha yanayo kutabisheni; anakuhangaikieni sana. Kwa Waumini ni mpole na mwenye huruma**}. Na kauli yake: **وَمَا أَرْسَلْنَاكَ إِلَّا رَحْمَةً لِلْعَالَمِينَ** {**Na wala hatukukupeleka isipokuwa uwe ni rehma kwa viumbe**}. Na kauli yake Mola Mtukufu: **النَّبِيُّ أَوْلَى بِالمُؤْمِنِينَ مِنْ أَنْفُسِهِمْ** {**Mtume ni bora zaidi kwa Waumini kuliko nafsi zao**}. Na kauli ya Mtume S.A.W:

**أَنَا أَوْلَى بكلِّ مُؤْمِنٍ مِن نَفْسِهِ؛ مَن تَرَكَ مَالًا فَلأَهْلِهِ، وَمَن تَرَكَ دَيْنًا أَوْ ضَيَاعًا، فَإِلَيَّ وَعَلَيَّ.**

"***Mimi ni bora mbora kwa kila Muumini zaidi ya nafsi yake, mwenye kuacha mali basi familia yake ni bora zaidi kurithi, na mwenye kuacha deni au watoto wadogo, basi hilo ni langu na jukumu langu***".

Hivyo Mtume S.A.W alikuwa ni baba bora mume bora babu bora rafiki bora, kwani alikuwa akisaidia familia na kuwatekelezea mahitaji yao, na alikuwa akitumia baadhi ya muda wake Mtume S.A.W kukaa na familia yake na kuwaletea furaha, ikiwa ni kuthibitisha kauli ya Mwenyezi Mungu: **وَعَاشِرُوهُنَّ بِالمَعْرُوفِ** {**Na**

**kaeni nao kwa wema**}. Na Mtume S.A.W anasema: **اسْتَوْصُوا بِالنِّسَاءِ خَيْرًا** "***Wausieni na waelekezeni wanawake kwenye mambo ya kheir***". Na kuali yake Mtume S.A.W: **اتَّقُوا اللهَ فِي النِّسَاءِ** "***Muogopeni Mwenyezi Mungu kwa wanawake***". Na akasema tena: **خَيرُكم خَيرُكم لأهلِه، وأنا خَيرُكم لأهلي** "***Mbora wenu ni yule mbora kwa familia yake, na mimi ni mbora wenu kwa familia yangu***".

Na Mtume S.A.W alikuwa ni baba mpole mwingi wa huruma, na alikuwa babu mwenye mapenzi sana na mkarimu, Anas Ibn Maliki R.A anasema: "*Sijawahi kumuona mtu yeyote mwingi wa huruma kwa watoto kuliko Mtume S.A.W*". na Mtume S.A.W alikuwa pindi anapoingia binti yake Fatuma R.A anamsimamia na kumbusu kwenye macho yake, na anamkarisha upande wake wa kulia, bali alikuwa akimuelezea baadhi ya mambo yake ikiwa ni kumheshimu na kumuamini.

Na Mtume S.A.W siku moja alipokuwa kwenye mimbari akitoa hutuba aliwaona wajukuu zake Hassan na Hussein *Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe kwao* wakiwa wanatembea huku wanachechemea, basi Mtume S.A.W aliteremka kwenye mimbari na kuwapokea na kuwabusu, na akasema:

**نَظَرْتُ إِلَى هَذَيْنِ الصَّبِيَّيْنِ يَمْشِيَانِ وَيَعْثُرَانِ، فَلَمْ أَصْبِرْ حَتَّى قَطَعْتُ حَدِيثِي وَرَفَعْتُهُمَا.**

"***Nimewaona watoto hawa wawili wanatembea wakiwa wanachechemea, sikuwez akusubiri isipokuwa nimekatisha mazungumzo yangu na kuwabeba***". Na Mtume S.A.W alikuwa anaswali akiwa amewabeba wajukuu zake, na anaposujudu anawashusha, pindi anaposimama anawabeba, ni upole ulioje na uzuri wake!

**HOTUBA YA PILI**

Shukurani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote, rehma na amani zimshukie Mtume wetu wa mwisho naye ni Mtume Muhammad sala na salamu ziwe kwake na kwa watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa kulinda kuishi vizuri na kufanya mazuri ni dalili ya uaminifu wa mwanadamu, na ni ishara ya uzuri wa dini yake na kigezo kizuri cha kuigwa

katika hilo, na mtu wa kupigwa mfano bora ni Mtume S.A.W ambaye alikuwa muaminifu kwa familia yake watu wake Maswahaba zake na watu waliomtangulia, pindi anapojiwa na mtu mzima kwa maana ya kikongwe alikuwa akimfanyia wema na kumkirimu, Bi Aisha R.A alipouliza katika hilo Mtume S.A.W akasema: "***Alikuwa anakuja wakati wa uhai wa Bi Khadija, hakika kutekeleza makubaliano na maelewano ni katika Imani***".

Na Mtume S.A.W anasema kwa watu wa Madina ambao walimuunga mkono na kumtetea:

**فَوَ الَّذِي نَفْسُ مُحَمَّدٍ بِيَدِهِ لَوْلَا الْهِجْرَةُ لَكُنْتُ امْرَأً مِنَ الْأَنْصَارِ، وَلَوْ سَلَكَ النَّاسُ شِعْبًا، وَسَلَكَتِ الْأَنْصَارُ شِعْبًا لَسَلَكْتُ شِعْبَ الْأَنْصَارِ، اللهُمَّ ارْحَمِ الْأَنْصَارَ، وَأَبْنَاءَ الْأَنْصَارِ، وَأَبْنَاءَ أَبْنَاءِ الْأَنْصَارِ.**

"***Ninaapa kwa yule ambaye nafsi ya Muhammad ipo mikononi mwake, lau isingekuwa huku kuhama basi mimi ningekuwa ni mmoja wa watu wa Madina, lau watu watatembea upande mmoja na watu wa Madina watatembea upande mwengine basi mimi ningetembea na watu wa Madina. Ewe Mwenyezi Mungu warehemu watu wa Madina na watoto wa watu wa Madina na wajukuu wa watu wa Madina***".

Na anasema kuhusu rafiki yake Abubakri:

**إنَّ أَمَنَّ النَّاسِ عَلَيَّ في صُحْبَتِهِ ومَالِهِ أبو بَكْرٍ، ولو كُنْتُ مُتَّخِذًا خَلِيلًا مِن أُمَّتي لَاتَّخَذْتُ أبَا بَكْرٍ، ولَكِنْ أُخُوَّةُ الإسْلَامِ ومَوَدَّتُهُ.**

"***Watu wa amani zaidi kwa urafiki wao na mali zao kwangu ni Abubakri, lau ningeteua rafiki katika watu wa umma wangu basi ningemteua Abubkri, lakini undugu wa Uislamu na mapenzi yake***". Na Mtume S.A.W hakuwa hivyo kwa watu wa nyumbani kwake na kwa Maswahaba zake tu bali alikuwa hivyo kwa watu wote.

Kama vile Mtume S.A.W alikuwa akiishi vizuri na familia yake pamoja na vipenzi vyake miongoni mwa Maswahaba, kwani siku ya vita vya Badri Mtume S.A.W anamkumbuka Al-Muutwiim Ibn Adawy, huyu mtu Mtume alipoingia Makka

akitokea safari yake ya Twaifu alikuwa pembezoni mwake, na akasema S.A.W: "***Lau Mutwiim angekuwa bado yu hai kisha akaniambia jambo kuhusu hawa mateka ya vita vya Badri basi ningewaacha kwake***".

Ni uzuri ulioje wa kuishi vizuri na familia ndugu majirani marafiki na watu wote, kwani Mtume Anasema: "***Mbora wao mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mbora wao kwa rafiki, na jirani bora mbele ya Mwenyezi Mungu ni yule mbora wao kwa jirani yake***".

Ewe Mwenyezi Mungu zilinde nchi zote za ulimwengu na ilinde Misri yetu na liinue jina lake ulimwenguni.

Na mwisho wa Dua yetu ni Alhamdulillahi Rabbilaalamedn wassalamu Alaykum warahmatullahi wabarakatuh